JULACE: Journal of University of Namibia Language Centre
Volume 4, No. 2, 2019 (ISSN 2026-8297)

# Uforensiki katika Ujumi wa Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Uchambuzi wa Riwaya ya "*Kikosi cha Kisasi*"

Neema Julius Luhwago[1]
*University of Dodoma*


## Abstract

*This paper aims to explore forensic aesthetics in Swahili literature showing how forensic induces the aesthetics in the Swahili novels. Forensic science emerged in the 19th century because of the development of science and technology. It has an impact on various fields of expertise such as law, chemistry, physics, biology and others for its effectiveness. Due to the misinterpretation of forensic in Swahili novels, most of the stakeholders of Swahili literary works such as Kezilahabi (1976), Hussein (1971) and Kimura (1991) emphasize that the authors of popular novels mimic the Western literary styles. Along with the negative attitude of various stakeholders of Swahili literature, the popular fictional Swahili novels still retain their status and are increasingly widespread in Swahili-speaking societies. This is due to the fact that these novels have the fascination of the phenomena introduced by the science and technology that clearly distinguishes itself around the world based on the aesthetic view of each society. This paper will dispel the negative stereotypes about the popular Swahili novels containing crime, romance and spying. In addition, it will introduce forensic aethetics as it relates to Swahili literature and emerges itself in Swahili novels such as Kikosi cha Kisasi.*

## Ikisiri

*Makala haya yanakusudia kuchunguza namna uforensiki unavyoibua ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili, sambamba na kuitambulisha taaluma ya uforensiki inavyojitokeza katika riwaya ya Kikosi cha Kisasi. Kutofahamikavyema kwa taaluma ya uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili, kumesababisha mtazamo hasi kwa wadau mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili kama vile Kimura (1991), Hussein (1971) na Kezilahabi (1976), waliotafiti na kuihakiki riwaya pendwa ya Kiswahili na kuiona kuwa ni riwaya isiyo na mafunzo yenye maadili kwa jamii, kutokana na maudhui yake ya ujambazi, mauaji, uhalifu, ujasusi, mapenzi na upelelezi kuelezwa waziwazi. Hali hii imesababishwa na uchache wa wanataaluma waliojihusisha na tafiti zinazohusu uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili. Hata hivyo, suala la uforensiki katika kuibua ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili halijashughulikiwa. Kutoshughulikiwa huko kunaendeleza mtazamo hasi wa kuziona riwaya hizi kuwa zimeiga utamaduni wa kigeni na hazina umuhimu katika jamii yetu, licha ya kuwa jamii yenyewe tayari imeshaathiriwa na utandawazi kutokana na*


[1] **Neema Julius Luhwago** is an assistant lecturer at the University of Dodoma in Tanzania. She pursued BA in Kiswahili Literature at the University of Dodoma, where she was also awarded a certificate of academic excellence. Moreover, she holds MA in Kiswahili Literature and she is currently pursuing PhD studies at the University of Dodoma. She has specialized in Aesthetics and Kiswahili Literature and she authored books on Theories of Oral Literature and Poems as well as several articles in aesthetics in Kiswahili Literature. Her research interests include Forensic Aesthetics in Kiswahili Literature. Email: neemajulius@ymail.com

*maendeleo ya sayansi na teknolojia.. Makala haya yatasaidia kuondoa mtazamo hasi uliopo juu ya riwaya pendwa ya Kiswahili na kuidhihiridha namna uforensiki unavyoibua ujumi katika riwaya pendwa ya Kiswahili hususani riwaya ya Kikosi cha Kisasi.*

**Utangulizi**

Dhana ya Uforensiki imetokana na neno la kilatini "f*orensis*" linalomaanisha "*forum*" yaani jukwaa la kujielezea (Bondergoard (2017). Aidha anaeleza maana ya uforensiki kuwa ni mahojiano ya kimahakama yanayohusiana na maarifa ya kisayansi yanayodadavua viashiria vya matendo ya kihalifu na kuleta ushahidi. Naye, Eckert (1992) ameelezea uforensiki kuwa ni taaluma ihusuyo kumtambua mhalifu kwa njia za kisayansi kama vile uchunguzi wa alama za vidole na vithibiti halisi kama vipimo vya kibiolojia, nywele, udongo na vitu vingine vilivyoachwa katika eneo ambalo uhalifu ulifanyika. Katika makala haya uforensiki umefafanuliwa kuwa ni taaluma ya upelelezi inayotoa ushahidi wa kisayansi na teknolojia aghalabu katika masuala ya kihalifu.

Taaluma ya uforensiki iliibuka karne ya 19 kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia (Eckert, 1992 na Coulthard, 2007) na aghalabu imekuwa ikijitokeza kwenye nyanja za sheria, sayansi ya kemia, fizikia, baiolojia na anthoropolojia kutokana na ufanisi wake. Aidha mwishoni mwa karne ya 20 uforensiki umeanza kujitokeza kwenye lugha, hususani katika sarufi ya lugha huku ukitumika kutambua, kubainisha, kuainisha na kutathmini uhalisi wa jambo kwa kutumia mbinu za sayansi na teknolojia yaani Isimu Forensiki (Malcolm 2017). Taaluma hii pia haikuishia hapo, kwenye fasihi inajitokeza katika mtindo wa usimulizi wenye ushahidi wa kiujumi unaojipambanua katika msuko wa matukio, lugha, usimulizi, muktadha na matumizi ya midia za kuona (coulthard 2007). Ushahidi huo wa kiujumi unatupeleka mbali zaidi katika maana ya ujumi kama inavyofafanuliwa na baumgarten (1973) kuwa ni ukamilifu wa hisi za akilini zinavyojipambanua katika sanaa ikiwemo fasihi.

Katika fasihi ya Kiswahili miongoni mwa tanzu ambazo uforensiki unajitokeza kwa uwazi ni utanzu wa riwaya pendwa, ambao lengo lake kubwa ni kuburudisha na kusisimua wasomaji. Maudhui yanayojitokeza katika utanzu huu aghalabu huwa ni upelelezi, uhalifu, ujasusi, mapenzi na mauaji.

Katika ufafanuzi wahistoria ya riwaya pendwa, Berg (1970) anaelezea historia ya riwaya ya upelelezi ya Uingereza iliyofumbata uforensiki kuwa ilianza kujitokeza miaka ya 1887 hadi 1927 ikiletwa na mwandishi mashuhuri Arthur Conan Doyle. Mwandishi huyu ndiye baba wa riwaya ya kipelelezi na katika kipindi hicho alikuwa na simulizi 60, hadithi fupi 56 na riwaya 4 ambazo zote zilihusisha wahusika Sherlock Holmes, Watson na wengineo katika ujenzi wa visa na matukio ya kihalifu yenye kuleta msisimko kwa wasomaji.

Halikadhalika tunapoitazama riwaya pendwa ya Kiswahili, tunaona kuwa imetokana na waandishi wa Kiswahili kuiga mtindo wa uandishi wa Doyle (ktj). Hili tunaliona pale Madumulla (2009) anapoielezea historia ya riwaya pendwa kuwa ilianza miaka ya 1957/8 ikifunguliwa mlango na Muhammed Said Abulla, ambaye aliathiriwa na mtunzi wa Kiingereza Doyle (KTJ). Madumulla anawataja waandishi wengine wa riwaya pendwa ya Kiswahili zenye mkondo wa kipelelezi ambao ni Faraji Katalambula na Aristablus Elvis Musiba.

Wataalam wa fasihi ya Kiswahili kama vile Kezilahabi (1979), Hussein (1971) na Kimura (1991) wanakosoa waandishi wanaoandika riwaya pendwa zanye mkondo wa kihalifu,

kipelelezi na kimapenzi kuwa na uigaji wa utamaduni na uandishi wa riwaya za kimagharibi. Hii ni kwa sababu matukio mengi yanayoelezwa katika riwaya hizi kuwa kama sinema zinazoonesha matukio ya kigeni, lakini kutumia wahusika, lugha na mandhari ya kitanzania.

Hoja hii inajipambanua wazi katika riwaya pendwa ya Kiswahili kuwa na maudhui yanayokiuka jadi ya Tanzania hususani katika kuelezea masuala ya mapenzi, mauaji, matusi ya nguoni na mengineyo ya faragha ambayo ujumi wa waswahili una namna yake ya kuyaelezea. Lakini katika riwaya pendwa masuala hayo yanawekwa waziwazi kama vikolezo na vivutio vyake.

Katika fasihi ya Kiswahili, utanzu wa riwaya pendwa ya Kiswahili, unajitokeza kuwa na matumizi ya uforensiki yanayoibua ujumi. Ni dhahiri kwamba ujumi katika sanaa haufungwi na vigezo vya kimaadili ili kudhihirisha uzuri wake. Schellekens (2007) ametoa sababu tatu zinazodhihirisha kuwepo kwa hitaji la kazi za kisanaa zinazoelezea masuala yasiyo ya kimaadili kubeba ujumi kama ifuatavyo:

i. Kazi ya sanaa inayopingana na maadili inaweza kuwa nzuri kwa sababu inatuburudishana hatulazimiki kufanya au kuiga yale yaliyowasilishwa;
ii. Kazi hizo huwa nzuri kwa kuwa hazina udhibiti au kukatazwa ambako tayari kupo ndani yetu;
iii. Ni nzuri kwa kuwa hukidhi haja ya kutaka kujua kwa undani juu ya yale tunayozuiliwa au kukatazwa na kanuni za jamii.

Kwa mantiki hiyo, mtazamo hasi juu ya riwaya pendwa ya Kiswahili umeibua ari ya udadisi kwa mwandishi wa makala haya juu ya uforensiki unavyojitokeza katika riwaya pendwa ya Kiswahili kwa kubainisha muktadha wa uforensiki, usimulizi wa kiforensiki, msuko wa matukio ya kiforensiki, mgogoro na matumizi ya lugha yanavyoibua ujumi katika riwaya ya Kikosi cha Kisasi.

**Mapitio ya Maandiko**

Mapitio haya yanahusu baadhi ya mijadala na tafiti mbalimbali zilizo fanyika kuhusu uforensiki, ujumi na riwaya pendwa ya Kiswahili. Mjadala huu utalenga kuonesha pengo la tafiti tangulizi ili kuonesha umuhimu wa makala haya sambamba na uhusiano wake na tafiti zilizo tangulia kufanyika.

**Uforensiki katika fasihi**

Bondergoard (2017) amejadili jinsi gani kazi ya fasihi inaweza kuwa ya kiforensiki. Kikubwa alichojadili ni kazi za fasihi zenye uforensiki zinavyoelezea kumbukumbu za matukio ya kihalifu na kuonesha namna ya kutambua umuhimu wa wahanga. Akisisitiza umuhimu wa msomaji kuwa mahiri kwenye mbinu za kiforensiki, anatofautisha uforensiki katika kazi ya fasihi na ule wa mahakamani. Ukurasa wa (5) anasema kuwa:

> “When the interpretation or presentation of evidence takes place in a literary work rather than in the courtroom, the evidence is, of course, interpreted according to a different logic. In the courtroom, forensics—as the art of the forum—tries to establish the facts about the event(s) in question and present them to the forum, potentially leading to conviction (or acquittal). In a forum surrounding a work of art the more general meanings raised by the

> particulars of the representation are exercised by the reader (see, for instance, Walsh 2007, 50).
>
> Wakati tafsiri au uwasilishaji wa ushahidi unapofanyika kwenye kazi ya sanaa badala ya mahakamani, bila shaka ushahidi huo unatafsiriwa kwa kutumia mantiki tofauti. Mahakamani, uforensiki kama sanaa ya uwasilishaji hujaribu kujenga hoja kuhusu matukio husika na kuwasilisha hoja hizo mahakamani ikiwa na uwezekano wa kumuhukumu mtu (au kumwacha huru). Kwenye jukwaa linalohusiana na kazi ya sanaa maana za jumla zaidi zilizoibuliwa kutokana na uwasilishaji maalum wa wahusika hufanywa na msomaji (Walsh 2007, 50). (Tafsiri yetu)

Hoja kubwa inayojitokeza katika ufafanuzi wake ni matumizi ya uforensiki katika fasihi. Aidha anatutazamisha namna uforensiki unavyoweza kujitokeza au kutumiwa katika kazi mbalimbali za fasihi na sanaa kwa jumla. Maelezo yake yanatupa mtazamo jumuishi kuhusu fasihi bila ya kutubainishia ni utanzu upi wa fasihi unaotumia uforensiki. Makala haya yanashughulikia uforensiki katika utanzu wa riwaya pendwa ya Kiswahili ili kusaidia kuziba pengo la kufinywa kwa mawanda ya uhakiki wa fasihi na sanaa kwa jumla.

Naye, Erickson (2014) katika kitabu chake cha *The basics of Forensic Investigation* anafafanua mambo ya msingi katika uchunguzi wa kiforensiki hususani ule unaohitaji ushahidi wa kimaabara. Ni lazima mchunguzi afahamu eneo la tukio, wahusika walipo eneo la tukio kama vile majeruhi, maiti, damu, nywele, viungo vya mwili n.k pamoja na vifaa vilivyokutwa eneo la tukio. Utafiti huu umetusaidia kuvifahamu baadhi ya vipengele vya uchunguzi wa uforensiki katika sayansi. Katika kuvifahamu vipengele vinavyoubainisha uforensiki katika sayansi bado mawanda ya fasihi na vipengele vinavyoubainisha uforensiki havijaoneshwa. Hivyo makala haya yanakusudia kuonesha ni kwa vipi fasihi hususani riwaya inaweza kutumia vipengele vya uforensiki katika ujenzi wake.

Kombo (2018) amethibitisha uwepo wa uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili kwa kuonesha matukio ya kiforensiki katika riwaya husika. Utafiti huu umesaidia kutambua kuwapo kwa uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili. Hata hivyo hakuonesha namna uforensiki unavyoibua ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili. Jambo hilo, lina sababisha kutoeleweka ipasavyo kwa taaluma ya uforenski jinsi inavyoibua ujumi wa riwaya ya pendwa ya Kiswahili. Hivyo basi makala haya yanaliziba pengo hilo la kimaarifa kwa kuchunguza namna matukio ya kiforensiki yanavyoibua ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili kupitia uchambuzi wa riwaya ya *Kikosi cha Kisasi.*

**Ujumi**

Kant (1970) anaeleza kuwa suala la ufahamu kwa njia ya hisia ndilo linaloamua ujumi. Akisisitiza kuwa uzuri ni jambo la kiulimwengu na huweza kupambanuliwa katika vitu kuwa ni kizuri au si kizuri kutokana na vionjo vya muhusika katika kazi ya sanaa. Utafiti huu unatupa kufikiri kwa kina jinsi suala la ujumi linavyojipambanua kiulimwengu. Pamoja na kuitazatama dhana ya uzuri kiulimwengu katika kazi ya sanaa, bado iko haja ya kuchunguza ujumi katika aina za sanaa. Hivyo basi, makala haya yatachunguza namna uforensiki unavyoweza kuibua ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili kama miongoni mwa utanzu wa sanaa unaojipambanua kupitia lugha.

Sanga (2012) amethibitisha uwepo wa ujumi katika riwaya pendwa ya Kiswahili kwa kuonesha namna ujumi unavyoibuliwa kupitia hisi na mguso unaotokana na matendo ya wanajamii. Utafiti huu umemsaidia mwandishi wa makala haya kuielewa dhana ya ujumi inavyojitokeza katika riwaya pendwa ya Kiswahili. Pamoja na hayo, bado utafiti wake haujaeleza kuwa mguso na hisi zinazoleta ujumi katika riwaya pendwa zinasababishwa na nini jambo linalosababisha kutoeleweka kirahisi kwa dhana nzima ya ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili. Hivyo basi, makala haya yanatumia uforensiki katika kuibua ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili ili kuweza kurahisisha uelewa wa dhana nzima ya ujumi katika riwaya pendwa ya Kiswahili kwa kutumia mfano wa riwaya ya *Kikosi cha Kisasi.*

**Riwaya Pendwa ya Kiswahili**

Madumulla (2009) anailezea riwaya pendwa ya Kiswahili kuwa ni aina ya riwaya iliyoletwa hapa Tanzania na mwandishi, Muhammed Said Abdulla, mwaka 1958, ambaye inaaminika kuwa aliiga baadhi ya mbinu kutoka kwa mwandishi mashuhuri wa Kiingereza, Arthur Conan Doyle (1850-1930). Akielezea mifano ya wahusika wake katika riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale kama vile Inspekta Seif na Najum wanaonekana kuwa sawa na Sherlock Holmes na Watson katika vitabu vya Doyle, ijapokuwa lugha, mavazi, mazingira na mazungumzo ya wahusika wake ni ya Kitanzania. Anawataja waandishi wengine wa riwaya pendwa ya Kiswahili baadhi yao wakiwa ni: Faraji Katalambullah, Aristablus Musiba, Ben Mtobwa, Eddie Ganzel, Hammie Rajab na John Simbamwene. Ufafanuzi huu, umemsaidia mwandishi kuielewa historia ya riwaya pendwa ya Kiswahili. Zaidi umempa tafakuri za kina mwandishi kuhusiana na uigaji wa uandishi wa riwaya za kimagharibi kujitokeza katika riwaya pendwa ya Kiswahili. Tunaweza kusema kuwa jambo hili limetokana na ujio wa maendeleo ya sayansi na teknolojia. Tafsiri ya uigaji iliyotolewa na Madumulla haikuhusisha suala la sayansi na teknolojia inayotokana na utandawazi. Hivyo basi, iko haja ya kutumia uforensiki katika kuihakiki riwaya pendwa ya Kiswahiliili kuthibitisha suala la muingiliano wa sayansi na teknolojia katika riwaya pendwa ya Kiswahili na siyo uigaji tu.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa riwaya pendwa ni mkondo unaojumuisha riwaya zote ambazo lengo lake kubwa ni kuburudisha na kusisimua wasomaji. Ameigawa riwaya pendwa katika tanzu nne kama ifuatavyo: Riwaya ya mahaba, riwaya ya uhalifu au ujambazi, riwaya ya upelelezi na riwaya ya ujasusi. Aidha mgawanyo wa aina hizo za riwaya pendwa umetumia kigezo cha kimaudhui. Mgwanyo huu unafinya utanuzi wa kihakiki wa riwaya pendwa ya Kiswahili na kuifanya idumae kwa kutoihakiki imeundwa kwa namna gani. Ufafanuzi wake unasaidia kuielewa riwaya pendwa ya Kiswahilina unalate mwanga wa kuweza kuihakiki kwa kina ili kurahisisha uelewekaji wake kwa jamii. Hivyo basi, iko haja ya kuchunguza uforensiki katika ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili ili kutanua mawanda ya kihakiki katika uga wa fasihi andishi.

Kimura (1991) anaeleza kuhusu riwaya ya upelelezi iliyoanza kuandikwa wakati wa ukoloni. Nchini Tanzania lianza baada ya mfumo wa polisi na mahakama kuanzishwa. Mbinu za upelelezi za kimagharibi zilianza kutumika kumpata mhalifu. Imani za kijadi zilizokuwa zikitumika katika kufichua mtu aliyetenda kosa hapo kabla katika hadithi zenye visa vya upelelezi zilianza kufifia na kuachwa kutumika. Kwa mtazamo wake matumizi ya sayansi na teknolojia yaliyopo sasa ni kuuacha utamaduni na asili, jambo ambalo linapingana na ukweli wa maisha kuwa jamii inakuwa na kupokea mabadiliko. Kwamantiki hiyo, utafiti wetu unakusudia kutumia uforensiki katika kuchunguza ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili ili kuondoa mtazamo hasi juu ya mabadiliko yaliyopo katika jamii.

Hivyo basi, kupitia tafiti na tahakiki mbalimbali zilizoelezewa hapo juu zimemjengea mwandishi uelewa wa kina kuhusiana na makala ya uforensiki katika ujumi wa riwaya pendwa ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, makala hayayanakusudia kuyaziba mapengo yote yaliyojitokeza sambamba na kutanua mawanda ya kihakiki katika uga wa fasihi ya Kiswahi hususani riwaya pendwa ya Kiswahili.

**Nadharia**

Makala haya yanaongozwa na nadharia ya Uhalisia. Mwasisi wa nadharia hii ni mwanafalsafa wa kijerumani Gustave Flaubert (1821-1880). Msisitizo wake ulikuwa katika fikra za mtu na ubainishwaji wa matatizo ya kijamii katika uhalisi wake (Wafula na Njogu, 2007). Nadharia ya Uhalisia iliibuka kwa lengo la kuipinga nadharia ya ulimbwende, ambayo ilionekana kushindwa kutatua matatizo ya watu na kuishia kuwa ni ndoto za akilini. Wafuasi wengine wa nadharia hii ni Karl Marx (1818-1883), Maxim Gorky (1868-1936), Gyorgy Lukacs (1885-1971). Wafula na Njogu (2007), wanafafanua baadhi ya misingi ya nadharia hii kama ifuatavyo:

i. Fasihi isawiri na kuelezea mambo kwa kuzingatia uhalisi wa maisha
ii. Fasihi ieleze mambo ya kihistoria yasababishayo mabadiliko chanya kwa jamii
iii. Fasihi itoe picha halisi ya jamii bila kuidunisha au kuitia chuku.
iv. Fasihi ioneshe matumaini kwa mwanadamu kuweza kushinda matatizo yanayomkabili katika mazingira yake.

Kutokana na uforensiki kutumia uhalisia wa masuala yanayochunguzwa, misingi ya nadharia hii itasaidia kuufafanua uforensiki kama unavyojitokeza katika riwaya ya Kikosi cha Kisasi. Aidha vipengele vya uforensiki kama vile muktadha, usimulizi, msuko wa matukio ya kiforensiki, mgogoro, wahusika na matumizi ya lugha yaliyopo kwenye riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* yamebainishwa.

**Uchambuzi wa Riwaya ya "*Kikosi cha Kisasi*"**

Uforensiki katika ujumi wa riwaya ya Kikosi cha Kisasi unaweza kuchambuliwa kupitia vipengele vingi. Baadhi ya vipengele hivyo ni Mgogoro, Msuko wa matukio, Muktadha, Wahusika na matumizi ya lugha. Katika makala haya mtafiti atatumia vipengelehivyo vitano ili kudhihirisha namna uforensiki unavyoibua ujumi wa riwaya ya *Kikosi cha Kisasi*.

**Mgogoro**

Mgogoro ni mvutano baina ya pande mbili au zaidi,mtu na mtu, kundi au hata mtu na nafsi yake. Aghalabu katika kazi yoyote ya kifasihi mgogoro huweza kujitokeza kwa lengo la kukuza kisa ambacho mtunzi anakielezea huku ukionesha chanzo cha matukio yatakayoendelea katika kisa hicho na pengine hata kudokeza mchakato wa suluhisho linalotarajiwa. Katika taaluma ya uforensiki mgogoro hutumika kama kiini au chanzo muhimu cha kuchunguza ili kuweza kujua ukweli wa matukio yaliyotendeka hususani yaliyosababisha mauaji, ujasusi, ujambazi na mengineyo yafafanayo na hayo.

Karika riwaya ya *Kikosi cha Kisasi,* mgogoro unaanza kujitokeza kati ya kundi la Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa nchi huru za Afrika (OAU) na wapinga mapinduzi wa Afrika wakiongozwa na makaburu waliojulikana kwa jina la White Power (WP) yaani nguvu ya weupe.Mvutano huu unasababishwa na uamuzi wa uongozi wa nchi huru za kiafrika kuamua kuchukua hatua ya kujikomboa kutoka katika ukoloni mamboleo uliokuwepo katika nchi nyingi za Afrika ukiendelezwa na makaburu ambao wamekita mizizi katika nchi ya Afika Kusini. Baada ya uongozi wa Nchi za Afrika kuanzisha harakati za kujikomboa na

kuwa na umoja wao ambao waliutumia katika kushauriana na hata katika nguvu za kijeshi. Wapinga mapinduzi ambao ni Makaburu au waliojulikana kwa jina la White Power (WP) yaani nguvu ya weupe, walianza mauaji ya viongozi wa Afrika ambao walikuwa ndio wakereketwa katika harakati za ukombozi wa nchi huru za Afrika. Jambo hilo liliamsha hasira kwa viongozi na serikali za nchi hizi za Afrika sambamba na vijana wazalendo wa kiafrika. Serikali za nchi hizo zilifanya upelelezi ili kujua ninini chanzo cha mauaji ya viongozi hao. Hii inajidhihirisha pale ambapo mwanyekiti anasema kuhusu kifo cha Ndugu Leon Fadaka, Mkuuwa ofisi ya wapigania Uhuru ya Dar-es Salaam aliyekufa kwa kulipukiwa na bomu lililokuwa limewekwa ndani ya kifurushi kilichotumwa kwake kwa njia ya posta kikitokea Kinshasa, Zaire. Mwanyekiti anasema:

> "Serikali ya Zaire ilijaribu kuchunguza juu ya jambohili, lakini haikufanikiwa…mwaka huohuo wajuzi kulitokea mauaji ya namna hiyohiyo hapa mjini Lusaka, baada ya Mkuu wa Ofisi ya Wapigania Uhru ya hapa mjini kupata barua kutoka mjini Paris, Ufaransa. Mara tu! Alipokuwa akifungua bahasha kukatokaea mlipuko ambao ulimwua hapohapo. Tukio hilo lililaaniwa vikali kote ulimwenguni.Lakini hakuna mtu au kikundi cha watu kilichokamatwa kuhusiana na kifo hicho bali lawama ziliwaanguakia makaburu na vibaraka wao kuwa ndio pekee wangeweza kuhusika na mauaji hayo" (ukurasa wa 06-07).

Pia kikaibuka kikundi cha vijana wazalendo wa Afrika ambao waliamua kupambana wao wenyewe bila ya miunganiko na serikali za nchi zao ili kuchunguza chanzo cha mauaji hayo kwa viongozi wapigania uhuru wa nchi za Afrika.Kikundi hiki kiliongozwa na kijana aliyejulikana kwa jina la Willy Gamba ambaye ni mpelelzi maarufu Afrika kutokana na ushujaa na uwezo wake wa hali ya juu katika taaluma hiyo ya upelelezi.Willy Gamba kutoka Tanzania aliungana na vijana wenzake wengine watatu waliojulikana kwa majina ya Kapteni Petit Osei kutoka Nigeria, Michael Degaro kutoka Msumbiji na Robert Sikawa kutoka Zambia (ukurasa wa 32-35). Vijana hawa waliongoza mapambano ya siri katika kufanya uchunguzi wa hali ya juu wa mauaji ya viongozi wazalendo na hatimae walifanikiwa kulipiza kisasi kwa kuteketeza mali za makaburu waliokuwa na kikundi cha wapinga mapinduzi wa nchi za AfrikaWhite Power (WP) yaani nguvu ya weupe sambamba na kuwa na wote walio husika (ukurasa wa 206-226).

Katika mgogoro huo tunaona kuwa *hisia* kama kipengele cha kiujumi kinajitokeza kikiwa kimejijenga katika moyo wa kizalendo uliopo kwa wapigania uhuru na vijana wanne wakiongozwa na kijana Willy Gamba katika kupambana na wapinga uhuru waliojulikana kwa jina la White Power. Hisia hizo zilizo zaa uzalendo na ujasiri zilisababisha vijana wapigania uhuru kutumia upelelezi wa kisayansi na teknolojia (uforensiki) ili kubaini kikundi cha wapinga uhuru wanaoshambulia viongozi wa nchi za jumuia ya wapigania uhuru wa Afrika.

**Muktadha**

Katika fasihi, muktadha hurejelea mahali na wakati kazi ya kifasihi imetendeka. Katika taaluma ya uforensiki muktadha ni kipengele cha muhimu sana kwenye uchunguzi wa tukio mauaji namna lilivyotendeka. Mazingira tukio lilipotendeka ni muhimu sana kwa kuweza kupata vithibiti kama vile vifaa vilivyotumika,udongo, damu,mwili wa marehemu ambao utafanyiwa uchunguzi wa kisayansi ili kubaini muhalifu au wahalifu.

Katika riwaya ya *Kikosi cha Kisasi,* miongoni mwa miktadha inaojenga tafakuri kiforensiki hasa ni ile ya matukio ya vifo vya viongozi wa wapigania uhuru wa nchi za Afrika. Baadhi

yao ni Raisi wa shirikisho la Vyama vya Wapigania Uhuru wa Kusini mwa Afrika Ndugu Edward Mongo kilichotokea huko Kinshasa, Zaire wakati wa usiku kwenye gari alillokuwa akitembelea kutegwa bomu ndani ya injini na kulipuka (ukurasa wa 04-05).Vilevile mazingira ya kifo cha Mkuu wa Ofisi ya Wapigania Uhuru ambayo ipo Dar-es Salaam Ndugu Leon Fadaka aliye uawa kwa bomu baada ya kupokea kifurushiambacho kilitumwa kwake kwa njia ya posta. Uchunguzi ulipofanyika iligundulika kuwa kimetoka Kinshasana Serikali ya Zaire ilijaribu kuchunguza jambo hili lakini haikufanikiwa (ukurasa wa 06). Sambamba na hilo ni mazingira ya hoteli ya TipTop huko Kinshasa, Zaire ambako Ndugu Meja Komba Matengo alikutwa ameuawa na Nalson Chikwanda mwakilishi wa wapigania uhuru wa huko Lagos Nigeria alipigwa risasi na mtu asiyejulikana (ukurasa wa 07-08). Hapa tunaona kuwa mazingiranawakati wa vifo vya viongozi hao wa wapigania uhuru yanajenga ari ya kidadisi kujua ni kwanini vilitokea na ninani aliyehusika.

> “Ndugu wanakamati, matukio kama haya, utaona ya kwamba yanatokea katika nchi zetu huru. Ingekuwa ni jambo jingine kama mauaji haya yangetokea kwenye uwanja wa mapambanoni…Suala sasa ni: tufanye nini? Kwa upande wangu naonelea ya kwamba inabidi tutafute kiini cha mauaji haya, kwani tukishapata kiini chake itakuwa rahisi kutafuta ufumbuzi” (ukurasa wa08).

Kutokana na muktadha au mazingira ya mauaji ya wapigania uhuru, *hofu* inatanda kwa wanajamii na wapigania uhuru kwa jumla. Hali hiyo ilisababisha vikundi vya wapigania uhuru kutafakari kwa kina njia madhubiti za kuweza kuwabaini watu wanao husika na mauaji hayo. Hofu hii iliitahadharisha jami na vikundi vya wapigania uhuru kuweza kutambua kuwa ni kwa namna gani vita yao katika kuleta ukombozi katika nchi za Afrika ilivyo.Vile vile iliwasaidia katika tafakari za njia stahiki katika kupambana ili kujikomboa.

**Msuko wa matukio**

Msuko wa matukio katika kazi yoyote ya kifasihi hurejelea namna visa vilivyo pangiliwa ili kuijenga kazi hiyo ya kifasihi na kuleta maana. Aidha, tunaweza kusema kuwa ni matiririko wa visa unaoijenga kazi ya kifasihi. Katika riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* tunaona jinsi ambavyo mfululizo wa matukio ya vifo vya viongozi wapigania uhuru yanaibua taharuki kwa serikali na vikundi vya wazalendo ambavyo nia yao nikutaka kupeleleza na kujua chanzo cha matukio hayo ya kikatili.

Kwenye (ukurasa wa06-08) tunaona kifo cha Ndugu Leon Fadaka aliyeuawa kwa bomu lililotegwa kwenye kifurushi, Nelson Chikwanda aliyepigwa risasi na mtu asiyejulikana,Meja Komba Mtengo aliyekutwa ameuawa katika chumba chake cha hoteli ya TipTop huko Kinshasa, kulipuliwa kwa ofisi ya wapigania uhuru huko mjini Nairobi nakusababisha vifo vya wafanyakazi watatu akiwemo ndugu Nene ofisa wa juu katika ofisi hiyo.Sambamba na tukio la kifo cha Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wapigania Uhru wa Kusini mwa Afrika Ndugu Edward Mongo huko Kinshasa,Zaire kwa kutegewa bomu kwenye injini ya gari lake alilokuwa akitembelea( ukurasa wa 05).

Mpangilio wa matukio hayo ndio ulioibua ari ya udadisi miongoni mwa vijana wazalendo na wapigania uhuru kutaka kujua chanzo cha mauaji ya viongozi hao na kutafuta njia ya kudhibiti vitendo hivyo vya kikatili na kulipiza kisasi kwa waliotenda uhalifu huo. Katika (ukurasa wa 06) mjumbe kutoka Kenya anasema:

> “Ndugu Mwenyekiti bado haijaelweka sawasawa kuhusu jambo tunalotakiwa tufanye. Kwa kweli jambo hili la kusikitisha sana na hata wakati natoka

> nyumbani niliacha baraza la Mawaziri limekaa kuzungumzia tukio hili. Kwa hiyo jambo tutakalozungumzia au kuamua hapa ndilo litakuwa msimamo wan chi huru za Afrika.Ndugu Mwenyekiti, tunaomba utuelezeekwa kinaganaga suala hili kusudi tuweze kulielewa sawasa na pindi tutoapo uamuzi uwe utakaolingana na matakwa ya nchi huru za Afrika"

Baada ya matukio ya vifo vya viongozi wa wapigania uhuru wanchi za Afrika. Tunaona kuanza kwa matukio ya upelelezi wa kina kuhusu vyanzo vya vifo hivyona mapambano ya kuwasaka wahalifu ambao ni wapinga mapinduzi ya nchi huru za Afrika walijulikana kama makaburu au White Power (WP) yaani nguvu ya weupe yalianza. Kikundi cha vijana shupavu na wenye uwezo wa hali yajuu katika taaluma ya upelelezi na kijeshi walianza kupambana nao kwa kulipua maeneo ambayo walipofanya uchunguzi walibaini kuwa ndimo ambamo wapinga mapinduzi waliishi na kufanya shighuli zao za kijasusi kwa siri na kibishara kwa wazi. Mfano biashara za gereji za magari, hoteli za kifahari na uwakala wa makampuni mbalimbali ya biashara za madini katika nchi ya Zaire na Afrika Kusini, Ufaransa, Marekani, Japan na Uingereza (kurasa wa 85-123). Kikundi cha vijana wapigania uhuru kilianza mashambulizi ya kuchoma moto gereji zote za makaburu na kuwauwa vibaraka wote na makaburu wenyewe ambao waliongoza ujasusi na uhujumu uchumi katika nchi za Afrika waliokuwa wamejikita nchini Zaire.

Hapa tunaona mapambano ya kivita yaliyosababisha kupatikana kwa ushindi kwa vijana wapigania uhuru dhidi ya wapinga uhuru yanaleta *taharuki* kubwa kwa jamii na ulimwengu kwa jumla. Uwezo wa kijeshi na ustadi wa kipelelezi uliotumika ili kuwabaini na kuwateketeza wapinga uhuru wa nchi za Afrika ni dhahiri kuwa ni wa kisayansi na teknolojia. Matumizi ya mabomu, bastola na vifaa vya kiteknolojia kama vile simu, vinasa sauti, kamera na vinginevyo vinadhihirisha hilo. Mapambano hayo yanadhihirisha matendo ya binadamu yanayojenga mtazamo wa kiujumi unaojipambanua katika mtu kukabiliana na mazingira yake ili kujiokoa.

**Wahusika**

Wahusika katika kazi yoyote ya fasihi ni binadamu au viumbe wasio binadamu kuvalishwa uwezo wa binadamu katika utendaji ambao ndio hutumika katika kutenda matendo mbalimbali yanayojenga kisa katika kazi ya fasihi. Katika riwaya ya *Kikosi cha Kisasi,* mtunzi ametumia wahusika binadamu wenye hulka na tabia tofauti tofauti kama vile, ujasiri, bidii, uzalendo, usaliti, ucheshi, mapenzi na kadhalika.

Katika riwaya ya *Kikosi cha Kisasi*wahusika waliotumika ni binadamu kama vile Willy Gamba, Kepteni Petit Osei, Michael Degaro, Chifu,Robert,Tete, Amanda, Charles,Jean, Pierre, Patron,Max, Fernand na wengineo ambao walivaa hulka tofautitofauti na kuwakilisha binadamu wa tabia tofauti tofauti kama za usaliti, ujasusi, ujambazi, ucheshi, ujasiri na mapenzi. Vilevila tunaona wahusika viongozi wazalendo wa kiafrika ambao waliamua kupigania uhuru wa nchi za Afrika bila ya ubaguzi wa rangi ambao waliongozwa na kijana Willy Gamba na wenzake wanne ambao walikuwa na ujuzi wa upelelezi wa hali ya juu yaani uforensiki katika kuchunguza mambo hususani mauaji, ujasusi na ujambazi. Vijana hawa walikuwa na ujasiri wa kukabiliana na changamoto zote katika kuhakikisha wana waangamiza wapinga mapinduzi wan chi za Afrika walikuwa wakiongozwa na makaburu akina Jean, Max, Patron,Fernand na wenzao (ukurasa wa 126-157).

Vile vile kuna wahusika wasaliti wa kiafrika ambao walikuwa vibaraka wa makaburu katika kuwapa siri za nchi za Afrika na namna serikali za Afrika zinavyofanya kazi. Katika hili

tunakutana na walinzi wa gereji zote za makaburu nchini Zaire, wafanya kazi wa hoteli zote za mjini Kinshasa, mawaziri wa serikali ya Zaire. Baadhi yao ni kama vile Kadima ambaye alikuwa ni kiongozi wa serikali ya Zaire katika kupigania uhuru ingawaje alikuwa msaliti na kibaraka wa makaburu wapinga mapinduzi yaani (WP) White Power nguvu ya weupe (ukurasa wa196-197). Vilevile Kasongo na Mulumba ambao walikuwa radhi kulipwa fedha na kusomea ujasusi na kuisaliti Afrika yao kwa kukubali kutumiwa na makaburu (ukurasa wa76-85). Tunaona Kasongo hata alipokamatwa na akina Willy Gamba na Robert hakukubali kusema siri za makaburu bali aliamua kujiua kwa kumumunya kipande cha peremende yenye sumu ambayo hutumiwa na majasusi kujiua pale wanapokuwa wamewekwa kizuizini na wanajua kuwa hawana namna yoyote ya kujiokoa:

> “Kasongo aliachama na kuzungusha zungusha ulimi wake halafu kitu kama peremende ndogo sana kikatokea mdomoni mwake naye akaanza kukimeza. Willy alipokiona tu, alimrukia kusudi asikimeze,lakini kwa bahati mbaya hakukiwahi. Kwani Willy alikitambua kitu hicho kuwa ni kidonge cha sumu ambacho hutumiwa hasa na majasusi wa hali ya juu sana wanaposhikwa, ili wajue wasiweze kutoa siri (ukurasa wa 85).

Vilevile,suala la mapenzi limejitokeza kwa baadhi ya wahusika kama vile Mwandi na Willy, Tete na Muteba na wengineo ambapo tunaona uhusiano huo wa kimapenzi uliweza kuwa msaada wa kukamatwa na kujulikana kwa baadhi ya taarifa za siri ambazo ingekuwa vigumu hususani kwa kikundi cha kupigania uhuru wa nchi za Afrika kuzifahamu.

Katika (ukurasa wa 566-110) tunamuona Mwandi anavutiwa na kijana Willy ambaye alifika katika Hoteli ya Memling na kumkuta binti Mwandi kama muhudumu eneo la mapokezi. Mwandi alivutiwa sana na Willy akaamua kufanya kila mbinu ili aweze kumpata Willy angalau kwa maongezi nae. Mvuto na msisimko wa hisia za kimapenzi alizokuwa nazo Mwandi kwa Willy, ulisababisha hata pale Makaburu wapinga mapinduzi na majasusi wa siri wa nchi za Afrika waliokuwa wamejificha katika nchi ya Zaire walipomtaka atoe taarifa ya orodha ya majina wageni waliongia katika hoteli ya Memling kwa siku zile hisia zilimtuma pengine wanataka hizo taarifa za orodha ya majina kwa nia mbaya hivyo hakuandika jina la Willy katika orodha ile.

Kitendo hicho kiliokoa maisha ya Willy ingawa baadae kilihatarisha maisha ya Mwandi hata aka uawa (ukurasa wa139-149).Vilevile uhusiano wa kimapenzi kati ya Tete na Muteba naTete kupendwa na Max kulisababisha Tete kujua siri zote za kijasusi sambamba na maeneo yao ya siri ya kufanyia ujasusi yaliyokuwepo katika gereji zao. Jmabo hili liliwasaidia sana akina Willy katika kupata habari za kina kuhusu ujasusi uliukuwa unaendelea nchini Zaire. Tunaona Tete akieleza hayo.

> “Max ananipenda sana mimi, amekuwa ananitongoza kwa muda mrefu sana…katika kutaka kujionyesha alivyo wa thamani kuliko Muteba na hao wengine amekuwa ananieleza mambo mengi sana. Anasema amewahi kuwa Meja wa jeshi la Ufaransa kabla ya kupewa kazi katika nchi mbalimbali zenye uhusiano na Ufaransa. Kipindi Fernand yuko likizo Ulaya yeye aliachiwa ofisi yetu kama Mkuu, ilipofika muda wakufunga ofisi aliniambia nisiondoke na wafanya kazi wengine waliondoka, tukabakia mimi nay eye tu. Kisha alifunga milango ya kutokea nje ya ofisi, akanijia na kuniamabi nimfuate…nilimfuata ingawaje kwa woga nilitaka nijue nia yake. Tulikwenda mpaka kwenye ofisi ya

> Fernand akaifungua tukaingia ndani akawa amenishika mkono tulikwenda mpaka kwenye ukuta nyuma ya meza ya Fernand akaniambia nisiogope kwani alitaka kuniaonesha mlango uliokwenda kwenye chumba cha siri ambako ndiko tungeweza kufanyia mazungumzo yetu. Alibonyeza kidude cha ukuta na ukaachana kumbe ni mlango wa kwenda chumba cha chini ya ardhi, Tukashuka ngazi kuingia chumba hicho ambacho kilikuwa na kila kitu…
> (Ukurasa wa190-191).

Katika kipengele hiki tunaona kuwa *hulka na tabia* mbalimbali kama vipengele vya kiujumi vinavyojipambanua katika mtu vinajitokeza. Miongoni mwa tabia za wahusika kama vile usaliti, mahusiano ya kimapenzi, uzalendo, ujasiri na zinginezo ndiyo huleta ladha ya maisha miongoni mwa wanajamii. Matukio mbalimbali ya kimauaji yanayotokea katika jamii huibua taharuki na huweza kuwa kichocheo cha kuchipuza miitikio tofauti tofauti kwa wanajamii.Miitikio hiyo huweza kuwa na matokea chanya au hasi kwa wana jamii. Ujasiri wa vijana wapigania uhuru ulileta matokeo chanya yaliyodhihirisha ushindi dhidi ya wapinga uhuru na vilevile ulizifungua fikra zao kujua kuwa jamii yao imevamiwa na majasusi wenye uwezo wa hali ya juu (uforensiki) katika kupambana.

**Matumizi ya Lugha**

Katika kazi za fasihi, matumizi ya lugha aghalabu hujipambanua kwenye vipengele tofauti tofauti kama vile tamahtali za semi, methali, vitendawili, nahau, misemo na vilevile lugha ya picha na taswira na kadhalika. Katika riwaya ya *Kikosi cha kisasi* lugha za picha zilizotumika nikama vile spea za magari ambayo ilitumiwa na kundi la majasusi wa pinga mapinduzi ya Afrika (WP) White Power wakimaanisha kundi la wapigania uhuru wa nchi za Afrika (OAU). Walitumia lugha hiyo ili kuficha ukweli wao kuwa wako kimkakati wa kuangamiza Waafrika wapigania Uhuru na waonekane kuwa ni wafanya biashara wa gereji za magari hivyo wanajishughulishana spea za magari.

Kwenye (ukurasa wa 176-177) tunaona Willy anaikamata barua ambayo ilikuwa imeandikwa kutoka kwa uongozi wa juu wa majasusi huko Afrika ya Kusini ikimtaka kiongozi wa White Power (WP) kuhakikisha anapokea spea kutoka kwenye makampuni ya watu wafuatao… iliendelea kutaja orodha ya viongozi wapigania uhuru wa Afrika ambao baadhi yao tayari walikuwa wameshakufa. Hapa majasusi walitumia lughahiyo ya spea ili kuendelea kuficha siri zao za kijasusi na mipango waliyokuwa nayo ya mauaji dhidi ya viongozi wa wapigania uhuru wa nchi za Afrika. Willy alipoisoma ilebarua ilikuwani kielelezo tosha kilicho wasaidia kwenyemapambano yao kujua mikakati ya majasusi imewekwaje.

Pia katika (ukurasa wa 74)…

> “Nimepata habari kutoka kwa wakala. Wanasema kuna spea zinawasili hapa toka Nigeria na ndege ya shirika la Ndege la Nigeria ambayo inaingia sasa tunapozungumza. Ni spea za aina mbili moja ni ndefu kama futi 5 inchi 10, nyeusi, imefunikwa suti nyeusi. Nyingine nayo ni ndefu futi 5 inchi 6 maji ya kunde imafunikwa na suti nyeusi vilevile. Hizi ni spea hatari sana. Lazima zikaangaliwe na kuona zinapelekwa duka gani ili iwe rahisi kuzinunua”.

Vilevile matumizi ya majina bandia, haya yalitumiwa na akina Willy na wenzake ili kuficha uraia wao na usalama wao ili wasijulikane kirahisi. Hili linajitokeza (ukurasawa 36-37).

> "…wao nao watakuwa wakitumia majina ya badia, Kapteni Petit Osei atakuwa akitumia jina la Ozu, Michael Degaro atakuwa akimia jina la Mike Kofi".

Pia matumizi ya lugha ya kiingereza, kinyanja, kilingala ni miongoni mwa lugha zilizotumiwa na wahusika katika riwaya hii (ukurasa wa 68,104,105,119, n.k).Vilevile matumizi ya maswali ya kidadisi yenye kumtisha muulizwaji. Maswali ya kipolisi yamejitokeza (ukurasa wa184-185) hapa Willy anahojiwa na polisi wakiwa wamemfuata kwenye hoteli aliyofikia ili kupata uhakika na uchunguzi wa nani amehusika na mauaji ya Mwandi.Mmoja wa mapolisi alimweleza Willy.

Hapa tunaona kuwa *idili* kama kipengele cha kiujumi kinajitokeza. Lugha ya picha, ishara na lugha za mazungumzo zilizotumika katika kikosi cha kisasi zilijiegemeza katika idili ambazo tayari zilikuwa zimejijenga miongoni mwa jamii na vikundi vya wapinga uhuru. Matumizi ya neno spea za magari kwa wapinga uhuru wakimaanisha wapigania uhuru ina dhihirisha idili zao za ufichaji wa shughuli za kijasusi walizokuwa wakiendelea nazo huku wakifanya kazi za gereji za magari. Vilevile matumizi ya lugha za kilingala, kiingereza, kinyanja na Kiswahili miongoni mwa vikundi hivi viwili ilikuwa ni sababu ya kujinasibisha na mazingira ya jamii husika ili kuepusha kutambulika kirahisi. Mtindo huo wa kujificha unajidhihirisha katika taaluma ya uforensiki.

**Hitimisho**

Kaposy (2018) anaelezea uforensiki wa kiujumi katika sanaa kuwa hujipambanua katikambinu za kiufundi, usimulizi, tamthiliya, uundaji na uharibifu wa sifa. Vipengele vingine ni: ukuzaji wa picha, alama, teknolojia ya uwasilishaji, uaminifu na umahiri. Fasihi kama kielelezo cha kisanaa kinachotumia lugha hususani riwaya ya *Kikosi cha Kisasi*, kupitia vipengele vya muktadha, mgogoro, matumizi ya lugha, wahusika na msuko wa matukio vimeweza kuubainisha uforensiki unaoibua ujumi katika riwaya hii ambao unajitokeza sawa na asemavyo Allison (2015) kuwa riwaya ya kiforensiki ni riwaya yenye visa vyenye kusisimua mno kutokana na motifu zake na msuko wa matukio yenye upeo mkubwa wa kifikra unaohitaji utulivu na uchunguzi wa kina kugundua mtuhumiwa au mhalifu.

Maelezo hayo yanashadadia uwepo wa ujumi unaojipambanua katika vipengele vya hisi, idili, hulka na tabia vinavyo dhihirika katika mtu na asili inayomzunguka. Riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* ni miongoni mwa riwaya zenye kujenga taharuki na msisimko wa hali ya juu kwa msomaji. Hii imetokana na msuko wa matukio yake yenye visa vya kusisimua vinavyo leta vionjo vya haja ya kutaka kujua zaidi. Pia Mgogoro, ujenzi wa wahusika wake na matumizi ya lugha na muktadha ambao matukio ya kijasusi, mauaji na mapambano yamefanyika unaibua ari na mshawasha zaidi wa kizalendo na hisia za kimapambano ambazo ndizo zinazoleta mvuto au uzuri yaani ujumi wa riwaya ya *Kikosi cha Kisasi.*Sambamba na matumizi ya vifaa vya kivita kama mabomu, bastola na na vinginevyo vya kiteknolojia kama vile simu, vinasa sauti, kamera katika harakati za upelelezi zinaidhihirisha taaluma ya uforensiki iliyopo kwenye jamii husika.

**Marejeleo**


Baumgarten, A. G. (1973). *Ästhetik als philosophie der Sinnlichen Erkenntnis Eine interpretation der "Aesthetica"*: Mit Teilweiser Wiedergabe des Lateinischen Textes Und Deutscher Übersetzung.

Jaffe, J. A. (1987). *Arthur Conan Doyle*. Boston: Twayne.

Kombo, F. (2018). *Uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka mzimu wa watu wa kale, Mhanga wa Ikulu na Kiu ya Haki* .Mastres dissertation, Chuo Kikuu cha Dodoma.
Kant, I., Guyer, P., & Mathew, E. (1970).*Critique of the power of judgment*, Cambridge.Cambridge University Press.
Kaposy, T., Eyal, W.& Thomas, K. (2018). *Mengele's Skull: The advent of forensic aesthetics*. Sternberg Press.
Kezilahabi, E. (1976). "Riwaya ya Upelelezi katika Fasihi ya Kiswahili" Katika *Mulika* na 46.Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: kur36-40.
Kimura, E. (1991). *Mabadiliko ya Kijamii na Riwaya ya Upelelezi.* Tanzania Institute for the Study of Language and Cultures of Asia and Africa.
Kothari, C. (2016). *Research methodology*: *Method and techniques* (toleo la 2), New Age
Madumulla**,** J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*: *Nadharia, historia na misingi ya Uchambuzi*, Dar es Salaam.Mture Education Publishers Ltd.
Malcolm, C. (2017). *Introduction to Forensic Linguistics: Language in Evidence*. London. Cenveo Publisher Services.
Mulokozi, M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam. Moccony Printing Press.
Musiba, E. A. (1979). *Kikosi cha Kisasi*. Dar es Salaam. Kilimanjaro Publications.
Sanga, A. (2012). "Ujumi katika Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka kwa Muhamed Sais Abdulla na Aristablus Elvis Musiba" Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma (haijachapishwa).
Schellekens, E. D. (2007). *Aesthetics and morality*. Continuum. London: Scheub.
Wafula, R. M., & Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi. The Jomo Kenyata Foundation.